



SWIS-H
STATEWIDE INFANT
SCREENING - HEARING



KWA NINI MTOTO WANGU ANAHITAJI KURUDI KWA KIPIMO CHA KUSIKIA TENA?

Watoto wachanga wengi huhitaji kurudi kupata vipimo vya kusikia tena.

Si lazima maana yake mtoto wako anapoteza uwezo wa kusikia. Inawezekana kuna sababu zingine kwa kipimo cha pili.

Sababu ya kawaida sana kuhitajika kupimwa kwa kurudia ni ugiligili (majimaji) au hali ya kuzuia ndani sikio la mtoto wako baada ya kuzaliwa.

Katika visa vingi kurudia tena kipimo cha kusikia kutafanywa kabla wewe na mtoto wako kutoka hospitalini.

Isipowezekana kufanya uchunguzi wakati upo hospitalini, utatolewa kurudia tena kipimo cha kusikia kwa mtoto wako kama mgonjwa wa nje au kwa mahali pa jamii pa eneo, punde tu baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini.

Mtu aliyekupa kifurushi hiki atakushauri kuhusu wakati na mahali pa uchunguzi wa kusikia kurudia tena utakapofanyika.

MATOKEO

Punde tu uchunguzi wa kusikia unapomalizika, matokeo yataelezwa kwako na kuandikiwa kwenye Kumbukumbu ya Afya ya Kibinafsi (Kitabu cha Bluu).

Kama kurudia uchunguzi wa kusikia hakuonyeshi matokeo wazi, mtoto wako ataelekezwa kwa kadirio ya uchunguzi wa uwezo wa kusikia na mtaalamu wa kusikia (audiologist). Mtaalamu wa kusikia ni mtaalamu wa vipimo vya uwezo wa kusikia.

Ni muhimu kugundua haraka iwezekanavyo jinsi mtoto wako anavyoweza kusikia ili wewe na mtoto wako muweze kupata ushauri sahihi na msaada.

KWA MAELEZO ZAIDI TAFADHALI UANGALIE TOVUTI IPO CHINI:

<http://www.health.nsw.gov.au/kids-families>

Habari za miadi/wasiliano wa eneo

Kwa ushauri wa afya wasiliana na *healthdirect Australia*
<http://www.healthdirect.gov.au/>
1800 022 222

